JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu: +255 26 2322761-5
Nukushi: +255 26 2324218
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz

BUNGE LA TANZANIA

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

## TAARIFA YA SPIKA KWA UMMA KUHUSU MABADILIKO YA TAREHE YA KUANZA KWA MKUTANO WA NNE WA BUNGE

Kwa mujibu wa Hoja iliyotolewa Bungeni na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu tarehe 26 Juni, 2026,** Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Tatu umepangwa kuanza siku ya **Jumanne tarehe 25 Agosti, 2026.**

Hata hivyo, kufuatia Taarifa ya **Baraza Kuu la Waislamu Tanzania** (BAKWATA) kuutangazia umma kuwa siku ya **Jumanne tarehe 25 Agosti, 2026 itakuwa ni Sikukuu ya Maulid,** Mheshimiwa Spika kwa Mamlaka yake chini ya **Kanuni ya 35 (4) na (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025** anapenda kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge na Umma wote wa Tanzania, kuwa mkutano wa Nne wa Bunge utaanza siku ya **Jumatano tarehe 26 Agosti, 2026 Saa 3:00 Asubuhi.**

Mabadiliko haya yamefanyika ili kutoa fursa kwa Waislam wote na Watanzania kwa ujumla kusheherekea Sikukuu ya Maulid inayotarajiwa kuadhimishwa Kitaifa siku ya Jumanne, tarehe 25 Agosti, 2026 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
**DODOMA.**

**17 Agosti, 2026**